Teacher.co.ke

# OPENER EXAMINATION: TERM 1 2024

## MWONGOZO WA KUSAHISHA KARATASI YA PILI

## KIDATO CHA 4

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

**1. UFAHAMU.**

a) Uhifadhi wa mazingira. (1x1=1)

b) Mabadiliko ya ghafla ya hali ya hewa (1x1=1)

c) Binadamu wa hapo awali angeweza kutabiri hali ya anga, wa sasa hawezi. Wa hapo awali aliweza kuhifadhi mazingira kwa kutokata miti kiholela, wa sasa hahifadhi. (2x1=2)

d) i) Kupanda miti akikata.
ii) Kutokata miti iliyochukuliwa kama chemchemi ya baraka. (2x1=2)

e) wakubwa serikalini kuharibu mazingira huku wakisikika wakihimiza athari za kukosa kuhifadhi mazingira. (2x1=2)

f) Wanasiasa maarufu kuvamia msitu mau na kujenga kiwanda cha majani chai.
Wengine kujenga viwanda vya kusagia mbao msituni mau.
Kukata miti katika misitu ya Aberdares na mlima Kenya. (3x1)

g) Kuondoa unafiki na tamaa. (1x1=1

h) Haramu – isiyo halali.
Anayejipalia makaa- anayejiumiza mwenyewe.
Ghadhabu – hasira. (3x1)

**2. UFUPISHO**

a) Fupisha aya nne za kwanza (alama 9)

i. Mataifa mengi hukumwa na baa la njaa.
ii. Kenya ni miongoni mwa mataifa hayo.
iii. Kenya huwa na hali inayoruhusu kilimo.
iv. Kenya huwa katika msururu wa mataifa ambapo uchumi wake unategemea kilimo.
v. Ukame umechangia umaskini kuzikumba jamii zinazofuga idadi kubwa ya mifugo.
vi. Wakazi wa mifugo imeathirika kwa ukosefu wa lishe.
vii. Watoto wamekumbwa na utapiamlo kwa uhaba wa chakula.
viii. Serikali ina changamoto ya kutafuta suluhu.
ix. Kiangazi ndicho kinachochangia uhaba wa chakula nchini
x. Hali ya njaa nchini ni kejeli
xi. Watu hukosa chakula kila baada ya miaka tano ambapo pia uchaguzi hufanyika.

Hoja zozote nane

b) Serikali inafaa kufanya nini ili kupambana na baa la njaa (alama 6)

i. Serikali iwafunze wakulima kuhusu hali ya hewa.
ii. Ipambane na wadudu wanaovamia mashamba ya mahindi katika bonde la ufa.
iii. Serikali iwahusishe wataalamu wa kilimo kuwasaidia wakulima ili tusihisi athari za njaa.
iv. Kutoketi kitako huku wakulima wakiteseka na kuhangaika.
v. Taasisi zenye wasomi wenye weledi watafute dawa za kuangamiza wadudu waharibifu.

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) insha (alama 1)

b) ha – ukanusho nafsi ya tatu wingi
wa – ngeli A-WA , nafsi ya tatu wingi

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

ku – ukanusho wakati uliopita
li – yambwa
lim - mzizi
a - kiishio (alama 3)

c) Gavana akijenga darasa shuleni atatuzwa (alama 2)

d) Vijuso vyao vimefura kabisa baada ya kuumwa na vijibwa (alama 2)

e) Nilifanya kazi shambani hadi jioni kisha nikatembea hadi nyumbani. (alama 2)

f) Shamirisho kipozi – nyimbo
Shamirisho kitondo – rais mteule (alama 2)

g) Wote hodari walimshangilia kiongozi alipowasili (alama 4)

| S (changamano) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| KN | | KT | | |
| W | V | T | N | $\overline{s}$ |
| Wote | Hodari | walimshangilia | kiongozi | alipowasili |

h) sokota (alama 2)
fungama

i) Kuonyesha maneno yenye maana sawa. Mfano, mzazi/mvyele (alama 2)
Kuandika tarehe. Mfano, 20/10/2022
Kuandika nambari ya kumbukumbu. Mfano, Kumb 1/02/22 *(Zozote 2)*

j) Angekimbia asubuhi – kishazi tegemezi (alama 2)
Angeishinda mechi hiyo – kishazi tegemezi

k) Mwalimu kijana - RN (alama 2)
aliyenunua lori juzi - RV
ametembelewa - RT
na wenzake - RH (4x ½)

l) Daktari atakuwa amemtibu kesho asubuhi. (alama 2)

m) Neema alimwita Riziki ili atume kwa mzee Busara lakini alishangaa na kutaka kujua kwa mzee Busara ni wapi. (alama 3)

n) ji – ma jina - majina (alama 2)
ya – ma yai - mayai
ja – ma jani - majani
ji – me jino – meno
# - ma. gari – magari *(zozote mbili)*

o)

Teacher.co.ke
Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes
Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

i) Katika mbuga la wanyama, amepatikana ndovu ambaye aliripotiwa kuwa ametoroka. / Katika mbuga la wanyama amepatikana ndovu aliyeripotiwa kuwa ametoroka. (alama 2)

ii) Walimu wana wajibu wa kuwafunza watoto wao vyema *au* ( alama 2)
Uwajibikaji wa walimu utapelekea kuwafunza watoto wao vyema

p) ingieni - wingi (alama 2)
darasani- mahali ndani
niwape – nafsi ya kwanza
ni – Kitenzi kishirkishi kipungufu (4x ½ )

q) Mtu auguaye huhitaji daktari (alama 2)

r) kata kamba
aga dunia
enda jongomeo
ipa dunia kisogo zozote 2, (2x ½ ) (alama 1)

**4. ISIMU JAMII**

a) Sajili ya kitaaluma/ mazungumzo rasmi/ sajili ya sekta ya afya/ sajili katika sekta ya afya/ sajili ya afya (alama 2)
Kwa sababu ni hotuba kwa wataalamu wa afya. Madaktari na wauguzi.

b) Sifa za sajili hii

i) Lugha hutegemea taaluma ya wataalamu husika.
ii) Lugha huwa rasmi. Kutumia lugha ya Kiswahili.
iii) Lugha huzingatia kanuni za kisarufi.
iv) Lugha huwa kavu kwa sababu hukwepa matumizi ya tamathali.
v) Lugha huwa ya adabu na heshima. Mfano, Hutaja vyeo kama vile Profesa, Daktari, mabibi na mabwana.
vi) Husheheni matumizi ya msamiati teule/ msamiati maalum wa afya.
vii) Mazungumzo huwa ya kitaaluma. Hakuruhusiwi uzushi, porojo au uongo.
viii) Lugha imesheheni matumizi ya takwimu. Mfano 50%, ½ ili kutoa ushahidi
ix) Huwa na mazungumzo yanayoegemea zaidi kwenye mantiki. Yaani mazungumzo hupangwa kwa kufuata utaratibu maalum
x) Aghalabu huwa kuna kuchanganya ndimi, ili kufafanua au kutilia mkazo dhana Fulani.
xi) Lugha huwa na sentensi ndefundefu ili kutoa maelezo ya kina.
xii) Lugha husheheni ushauri
xiii) Huwa lugha ya tasfida, ili kufisha makali ya msamiati.
xiv) Matumizi ya utohozi/ msamiati wa kutoholewa, ili kuakisi maenedeleo ya kiteknolojia katika sekta ya afya. Mfano, eksirei, stretheskopu
xv) Kuna matumizi ya takriri/uradidi, ili kusisitiza mambo muhimu

*Hoja zozote nane.*

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Tanbihi: Lazima mwanafunzi atoe mfano au atoe ufafanuzi ili atuzwe alama 1.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes